**TUME YA KIKRISTO YA HUDUMA ZA JAMII (CSSC)**
**KANDA YA KASIKAZINI**

**MTIHANI WA KUJIPIMA KABLA YA MTIHANI WA TAIFA**
**KIDATO CHA NNE**
**KISWAHILI**
MWONGOZO WA USAHIHISHAJI NA MGAWANYO WA ALAMA KWA KILA SWALI

**1. ALAMA 1@ KIPENGELE =10**

| i. | ii. | iii. | iv. | v. | vi. | vii. | viii. | ix. | x. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | A | E | C | A | E | B | C | D | C |

**2. ALAMA 1@ KIPENGELE =06**

| ORODHA A | i. | ii. | iii. | iv. | v. | vi. |
|---|---|---|---|---|---|---|
| ORODHA B | C | F | G | B | A | H |

**3. (a).Alama 1@ kipengele x4=04**

i. Uhusiano baina ya wazungumzaji . mfano. Baba na mama , mwanafunzi na mwalimu, mwanafunzi na mwanafunzi mwenzake
ii. Mada ya mazungumzo . mfano. Masom kwa wanafunzi, tiba, biashara, michezo nk
iii. Muktadha wa mazungumzo . mfano Kanisani, Gulioni, nymban,
iv. Malengo au madhumuni ya mazungumzo. Mfano Kuonya, kuelimisha, kutoa mawaidha au kushauri nk
v. Utanzu wa mazungumzo. Mfano. Risala, Hotuba nk
vi. Mila na desturi

Mtahiniwa asipotoa mifano apewe nusu alama (0.5)

(b). **Alama 1@ kipengele x 5 =05**

i. Chajio-uhulutishaji / udondeshaji wa maneno
ii. Kionambali – Uambatanishaji wa kitenzi na kielezi / kuangalia kazi ya kitu
iii. Kidoletumbo -ufananishaji wa umbo la kitu/kufananisha umbo la kitu / uambatanishaji
iv. Babaika -uradidi usio kamili / uradidi nusu
v. Daktari – Utohoaji

4. (a) Alama 1@ x4=04

i. Kichwani
ii. Vinasa sauti/ tepu rekoda
iii. Maandishi
iv. Picha za filamu
v. Vyombo vya kisasa kama vile Kinyonyi, CD, DVD
vi. Tarakilishi (kompyuta), simu za mkononi
vii. Intaneti
viii. Makazi

NB : mwanafunzi akiandika njia zingine tofauti na hizi ambazo zinahusiana na swali apewe alama .

**( b). Alama 1@x5=05**

i. Kuteuliwa kuwa lugha ya taifa
ii. Kutumika kutolea elimu nchini
iii. Kutumika katika shughuli za serikali kama Bungeni na mahakaman

iv. Kuanzishwa kwa vyombo mbalimbali vya kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili
v. Kutumika katika vyombo vya Habari


5. Mtahiniwa azingatie vipengele vifuatavyo katika kuandika kumbukumbu ya mkutano wa pili
   i. Kichwa cha kumbukumbu kioneshe lengo la mkutano, mahali mkutano unakofanyika, tarehe na muda
   ii. Mahudhurio : orodha ya waliohudhuria na wasiohudhuria
   iii. Ajenda ya mkutano
   iv. Kufungua mkutano
   v. Kusomwa kwa muhtasari wa kikao kilichipita na kuthibitisha
   vi. Yatokanayo na mkutano uliopita
   vii. Mengineyo
   viii. Kufunga mkutano

**Kichwa alama 2 na alama 1 kwa vipengele vingine jumla =9**

6. **(a) Alama 1@ x4 =04**
   i. Ngeli ya kwanza **(YU – A -WA)**
   ii. Ngeli ya kumi **( YA - YA)**
   iii. Ngeli ya tatu **(LI – YA)**
   iv. Ngeli ya nane **(I - I)**

   **(b). Alama 1@x5=05**

   Balozi wetu alikuwa mtu jasiri sana




7. Mtahiniwa azingatie mambo yafuatayo katika uandishi wa tangazo
   **i.** Kichwa cha tangazo kibebe kiini cha tangazo **(Alama 2)**
   ii. Anuani au mawasiliano **(Alama 01)**
   iii. Matumizi ya picha michoro na vielelezo **(Alama 03)**
   iv. Lugha yenye ushawishi
   v. Tangazo liwe fupi na la kueleweka
   vi. Matumizi ya lugha fasaha na yenye mvuto
   vii. Kutumia watu maarufu

   **Alama 1@x3=03**

8. (a) Alama 1@x4= 04
   i. Makosa ya kuongeza vitamkwa mahali ambapo hapastahili mfano. Tunalimaga, huwaga
   ii. Makosa ya kimuundo mfano mdogo mtoto analia sana
   iii. Makosa ya upatanisho wa kisarufi mfano chiti hiki kibovu
   iv. Makosa ya tafsiri sisisi mfano osha uso badala ya nawa uso
   v. Makosa ya kuacha baadhi ya vitamkwa mfano Baba ameondoka kazini badala ya Baba ameondoka Kwenda kazini
   vi. Makosa ya kimsamiati mfano wakilisha badala ya wasilisha
   vii. Makosa ya kimatamshi mf. Masiwa badala ya maziwa

   (b). **Alama 5**

   (i) UCHAGUZI MKUU 2020 (Alama 2)

   (ii). Kila baada ya miaka mitano (Alama 1)

(iii). Awe amejiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapiga kura na awe na umri wa miaka kumi na nane (18) na kuendelea (Alama 1)

(iv). Ndiyo: -Hutupatia viongozi walio bora na wenye uwezo wa kuwawakilisha wananchi pia kuwa na demokrasia iliyosimama yenyekuleta usawa miongoni mwa wanajamii(Alama 1)

9. Utangulizi
   - Mtahiniwa aeleze maana ya matatizo . Matatizo ni changamoto mbalimbali zenye kuikabili jamii.
   - Kiini – mtahiniwa akubali usemi huo kwa kuonesha jinsi wanajamii wnavyosababisha matatizo yanayoikumba jamii yao, kw kuzingatia vitabu vya riwaya walizosoma.

   **RIWAYA YA WATOTO WA MAMANTILIE**
   - Msanii anaonesha jinsi mwalimu Chikoya alivyosababisha tatizo la ukosefu wa elimu kwa kuwafukuza Watoto wa Mamantilie Peter, Zitta na Musa shule.
   - Masta Baroni amesababisha tatizo la biashara ya madawa ya kulevya kwa kuwahusisha Watoto katika biashara haramu Peter na Musa wakafungwa jela kwa ajili yake.
   - Mwandishi anaonesha tatizo la umaskini ambalo limesababishwa na wanajamii wenyewe . mfano Mzee lomolomo

   **RIWAYA YA TAKADINI**
   - Tatizo la ubaguzi na unyanyasaji limesababishwa na wanajamii wenyewe kwa mfano, mtunzi anaonesha jinsi jamii ya takadini walivyombagua Takadini tangu utoto wake . Rejea Mzee Makwati na Nhamo.
   - Matatizo ya kifamilia yanasababishwa na wanajamii wenyewe . mfao mzee Makwati anaifarakanisha familia yake kwa kushikilia mil ana desturi potofu.
   - Ugomvi na migogoro ya kifamilia kutokana na mila potofu ya ndoa za mitara , rejea familia ya Mzee Makwati na Mtemi Masasa .

   **RIWAYA YA JOKA LA MDIMU**
   - Tatizo la hali ngumu ya Maisha kwa wananchi wa kawaida katika nchi ya mindule . Tatizo hili linasababishwa na uongozi uliopo . Rejea kwa Zito na Amani.
   - Tatizo la rushwa nalo limesababishwa na viongozi kwa kuendekeza rushwa . Rejea kwa Brown Kwacha
   - Tatizo la urasimu linasababishwa na wanajamii wenyewe . Msanii anaonesha ukiritimba wa vuingozi katika kuhudumia wananchi . Rejea mazungumzo ya Brown Kwacha na Amani.

   Mgawanyo wa Alama .
     - **Utangulizi=02**
     - **Kiini =2x6=12**
     - **Hitimisho =1**

10. Mtahiwa anatakiwa kueleza jinsi lugha ilivyomalighafi ya mwandishi kwa kutoa hoja tatu kwa kila riwaya mbili alizosoma.

**Utanguluzi.**

Mtahiwa aeleze maana ya lugha kifasihi kuwa ninamna ambapo mwandishi wa kazi ya fasihi yeyote anavyotumia lugha kuisuka kazi yake. Malighafi ni mali au hazina. Mwandishi ni mtu yeyote anayetumia muda wake mwingi kuzungumza na jamii yake kwa njia ya maandishi.

**KILIO CHETU**
- Mtunzi ametumia taswira mbalimbali kwa lengo la kujenga kazi yake. Ametumia taswira ya dubwana akimaanisha ugonjwa hatari wa UKIMWI.
- MISEMO Mfano wembamba wa reli treni inapita akimaanisha jinsi Watoto wadogo wanajihusisha kwenye mapenzi katika umri mdogo
- Methali. Mfano “asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu; akimaanisha umuhumu wa elimu ya jinsia kwa Watoto(rejea kwa MJOMBA na mama Suzy)

**Tamathali za semi kama vile:**

- Tashibiha . mfano: "mbona una kuwa mgumu kama mpingo?"
- Sitiari mfano; "huyo kinyago wako anakimbia nini?"

**PENZI KITOVU CHA UZEMBE**

- Methali mfano "penye nia pana njia"
- Taswira mfano kijito , vijito, mto, jito na bahari akimaanisha jinsi matatizo yanavyoanza taratibu mwishowe huw makubwa
- Tamathali za semi mfano tashibiha "vumbi jekundu kama ugoro wa subiana?..."

**ORODHA**

- Kuna matumizi ya misemo na nahau mfano: Shuga dadi wanaume wenye umri mkubwa wenye tabia ya kuwa na mahusiano na Watoto wadogo

"Furaha anavuna mbegu ya kifo aliyoipanda"akimaanisha kupata kitu kutokanan na matendo yake

- Matumizi ya msimu(lugha ya mitaani) mfano mazungumzo kati ya Kitunda na Furaha
- Matumizi ya tamathali za semi. Mfano tashibiha "yeye ni kama punda wa Kijiji…"
- Matumizi ya sitiari. Mfano "nyie mbu wadogo….."

**Mgawanyo wa alama: utangulizi (Alama 02)**
**Kiini: alama 02kila hoja. Hoja 3X2X2=12**
**Hitimisho alama 01**

11. Mtahiniwa anatakiwa kuonesha jinsi mshairi alivyokuwa kiongozi wa jamii kwa kutumia riwaya zao

**Utangulizi.** Mtahiniwa aeleze maana ya mshairi na kiongozi kama ifuatavyo:

Mshairi ni mtu yeyote mwenye ujuzi wa kutunga, kuimba na kughani mashairi. Kiongozi ni mtu yeyote mwenye jukumu la kuongoza jamiii.

**MALENGA WAPYA**

- Mshairi ameweza kupiga vita ukoloni mamboleo. Kwa mfano shairi la "Nipatieni Dawa" na "sokomoko Baharini"
- Mshairi amesisitiza kuhusu umuhimu wa kuinua uchumi wa nchi yetu. Mfano shairi la " Tuyazingatie Haya"
- Mshairi amepiga vita kuhusu matendo mabaya yanayofanywa na wanajamii. Mfano shairi la "Hisani Hulipwa"

**WASAKATONGE**

- Mshairi ni kiongozi wa jamii kwasababu ameweza kupiga vita matabaka katika jamii. Mfano shairi la Wasakatonge, Kansa na Vinyonga
- Mshairi amepiga vita kuhusu mmomonyoko wa maadili katika jamii mfano shairi la Jiwe si Mchi na shairi la Mamantilie
- Ni kiongozi wa jamii kwasababu mshairi amepiga vita kuhusu umaskini na kuelekeza watu kufanya kazi kwa bidii. Mfano shairi la Mvuja Jasho

**Mgawanyo wa alama**
**Utangulizi (alama 02)**
**Kiini. Alama 02 kila hoja 3X2X2=12**
**Hitimisho alama 01**